

Tathmini ya Hatari ya Kifua Kikuu kwa Watu Wazima ya Kaunti ya Los Angeles

- Tumia zana hii ili kuwatambua **watu wazima** wasio na dalili kwa ajili ya vipimovya maambukizi ya Kifua Kikuu
- Vipimo vipywa vinapaswa kuchukuliwa tu kwa watu ambao hapo awali walipima na kuonekana hawana maambukizi, na wana sababu **mpya** za hatari tangu tathmini iliyopita.
- Kwa dalili za Kifua Kikuu au eksirei ya kifua isiyo ya kawaida inayoendana na ugonjwa wa Kifua Kikuu → Chunguza ugonjwa wa Kifua Kikuu uliopo

Tathmini kamili ya ugonjwa wa Kifua Kikuu uliopo hujumuisha: uchunguzi wa wa dalili, eksirei ya kifua, na kama imeonyeshwa uchunguzi wa AFB ya makohazi, ukuzaji wa bakteria na upimaji wa ongezeko la asidi ya nukleiki. Kipimo cha kuingiza tuberculin kwenye ngozi hakijaona maambukizi ya kifua kikuu au kupima utokaji wa gama ya interferon hauondoi ugonjwa wa Kifua Kikuu uliopo.

Chagua visanduku sahihi vya mambo hatarishi hapa chini.

Upimaji wa maambukizi ya Kifua Kikuu umependekezwa iwapo visanduku vyovyote kati ya 4 vya hapa chini vimechaguliwa.

Ikiwa majibu ya kipimo cha maambukizi ya Kifua Kikuu yanaonyesha kuna maambukizi na ugonjwa wa Kifua Kikuu uliopo umekataliwa, matibabu ya maambukizi ya Kifua Kikuu yanapendekezwa.

Kuzaliwa, safari, au ukazikatika nchi yenye kiwango kikibwa cha Kifua Kikuu kwa angalau mwezi 1

- Hii ni pamoja na nchi zingine isipokuwa Marekani, Kanada, Australia, New Zealand, au nchi za Magharibi na Kaskazini mwa Ulaya
- Iwapo rasilimali zinahitaji kipaumbele ndani ya kundi hili, wape **kipaumbele** wagonjwa wenye angalau hatari moja ya kiafya kwa ajili ya uendelezaji (angalia Kijitabu ili kupata orodha)
- Kupima utokaji wa gama ya interferon hupendelewa zaidi ya Kipimo cha Kuingiza Tuberculin kwenye ngozi kwa watu ambao hawajazaliwa Marekani wenye umri wa ≥ 2

Upungufu wa kinga, sasa au iliyopangwa

- Maambukizi ya VVU, mtu aliyepandikizwa viungo vya mwili, kutibiwa kwa kutumia adui wa TNF-alpha (kwa mfano, infliximab, etanercept, wengine), steroidi sawa na prednisone ≥ 15 mg/siku kwa mwezi ≥ 1) au dawa nyingine ya kudhoofisha kinga.

Kutangamana kwa karibu na mtu mwenye maambukizi ya Kifua Kikuu wakati wowote

- Vituo vya Kudhibiti na Kupambana na Magonjwa vinaonyesha kwamba uchunguzi wa watu waliotangamana na mgonjwa na matibabu kwa watu wenye maambukizi ni sehemu muhimu ya mkakati wa Marekani wa kutokomeza Kifua Kikuu.

Historia ya kukosa makazi au kufungwa

- Kikosi Kazi cha Huduma ya Kinga cha Marekani (USPSTF) kinapendekeza watu walio katika hatari kubwa ya kuambukizwa Kifua Kikuu kutokana na ongezeko la hatari ya kuambukizwa ikiwemo watu ambao wameishi katika mazingira ya hatari yenye mkusanyiko wa watu (kwa mfano; nyumba za watu wasio na makazi na vituo vya kurekebisha tabia)

Kumbuka; hakuna vipimo vya Kifua Kikuu vilivyoonyeshwa kwa sasa.

Mtoa huduma: _____

Tarehe ya Tathmini: _____

Jina la Mgonjwa: _____

Tarehe ya kuzaliwa: _____

(Weka stika hapa kama inafaa)

Tazama **Mwongozo wa Mtumiaji wa Kaunti ya Los Angeles wa Tathmini ya Hatari ya Kifua Kikuu kwa Watu Wazima** kwa taarifa zaidi kuhusu kutumia zana hii.

Umetoholewa kwa ajili ya matumizi ya LAC kutoka kwenye Tathmini ya Hatari ya Kifua Kikuu ya California unapatikana kwenye ukurasa wa WATOA HUDUMA kwenye www.ctca.org ili kuhakikisha kwamba unakuwa na toleo jipya zaidi tembelea <http://publichealth.lacounty.gov/tb/providertoolkit.htm>

